/

# HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA

## TENDA NA. LGA-007/2023-2024/HQ/NC/02

**ZABUNI ZA UPATIKANAJI WA MAWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA KATIKA VYANZO VYAKE MBALIMBALI**

**TAREHE: 20/05/2023**

# KABRASHA LA ZABUNI(TENDER DOCUMENT)

## YALIYOMO

Dibaji ........................................................................................ **Error! Bookmark not defined.**

**VIFUPISHO** ........................................................................................................ iii

SEHEMU YA KWANZA: MWALIKO WA ZABUNI ........................................................ 1

SEHEMUYA PILI: MAELEKEZO KWA WAZABUNI........................................................ 4

SEHEMU YA TATU: LOHODATA YA ZABUNI (LDZ) .................................................. 24

SEHEMU YA NNE; JEDWALI LA MAHITAJI NA BEI.................................................... 28

SEHEMU YA TANO: MAELEZO YA VIGEZO MSAWAZO VYA KIUFUNDI ........**Error! Bookmark not defined.**

SEHEMU YA SITA: AGIZO LA UNUNUZI (ALU)............. **Error! Bookmark not defined.**

VIGEZO NA MASHARTI YA AGIZO LA UNUNUZI:........ **Error! Bookmark not defined.**

JEDWALI LA MAHITAJI NA BEI ....................................... **Error! Bookmark not defined.**

SEHEMU YA SABA: MASHARTI YA JUMLA YA MKATABA (MJM)**Error! Bookmark not defined.**

SEHEMU YA NANE: MASHARTI MAALUM YA MKATABA (MMM) AU AGIZO LA UNUNUZI (ALU).................................................................. **Error! Bookmark not defined.**

MASHARTI MAALUM YA MKATABA.............................. **Error! Bookmark not defined.**

SEHEMU YA TISA: FOMU .................................................................................... 39

SEHEMU YA KUMI: UADILIFU ............................................................................. 48

AHADI YA MTOA HUDUMA KUHUSU SERA DHIDI YA RUSHWA, KANUNI ZA MAADILINA PROGRAMU YA UKIDHI .............................................................. 53

# VIFUPISHO

| | | |
|---|---|---|
| **ALU** | - | Agizo la Ununuzi |
| **MJM** | - | Masharti ya Jumla ya Mkataba |
| **MMM** | - | Masharti Maalum ya Mkataba |
| **MZ** | - | Mwaliko wa Zabuni |
| **NSZ** | - | Nyaraka Sanifu za Mwaliko wa Zabuni |
| **PPA** | - | Sheria ya Ununuzi wa Umma, Sura ya 410 |
| **TANePS** | - | Mfumo wa Kitaifa wa Ununuzi kwa njia ya Mtandao |
| **TIN** | - | Namba ya Utambulisho wa Mlipa Kodi |
| **TJU** | - | Tangazo la Jumla la Ununuzi |
| **TN** | - | Taasisi Nunuzi |
| **UZM** | - | Ushindani wa Zabuni Kimataifa |
| **UZT** | - | Ushindani wa Zabuni Kitaifa |
| **VAT** | - | Kodi ya Ongezeko la Thamani |

# SEHEMU YA KWANZA: MWALIKO WA ZABUNI

**HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA**

**Namba ya Zabuni**: LGA-007/2023-2024/HQ/NC/01

# TANGAZO LA ZABUNI YA KUWAPATA MAWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA KATIKA VYANZO VYAKE MBALIMBALI

## TAREHE: 20/05/2023

1. Halmashauri ya Wilaya ya Arusha inapenda kualika zabuni kutoka kwa watu Binafsi, Makampu*ni, Ushirika, Taasisi au Vikundi* vya watu vilivyosajiliwa k*isheria wenye nia, uwez*o na uzoefu wa kufanya kazi ya uwakala wa kukusanya mapato katika vyanzo vyake mbalimbali katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kwa kipindi cha kuanzia tarehe **01.07.2023** hadi tarehe **30.06.2024** kama ilivyojionyesha katika jedwali hapa chini.

| | **CHANZO CHA MAPATO** | **NAMBA YA ZABUNI** |
|---|---|---|
| | Ushuru wa madini ya Ujenzi geti la Mbutuni kata ya Oljoro | **LGA/007/2023/24/HQ/NC/02 LOT 1** |
| | Ushuru wa Moram Nyeupe Oldonyosambu | **LGA/007/2023/24/HQ/NC/02 LOT 2** |
| | Ushuru wa Masoko ya Mirongoine, Oldonyowas, Ngaramtoni na Kisongo | **LGA/007/2023/24/HQ/NC/02 LOT 3** |
| | Ushuru wa Maegesho | **LGA/007/2023/24/HQ/NC/02 LOT 4** |
| | Ushuru wa choo Soko la Ngaramtoni na Oldonyowas | **LGA/007/2023/24/HQ/NC/02 LOT 5** |
| | Ushuru wa Moram Kisongo | **LGA/007/2023/24/HQ/NC/02 LOT 6** |
| | Ushuru wa Mkaa na mazao ya misitu geti la Kisongo | **LGA/007/2023/24/HQ/NC/02 LOT 7** |
| | Ushuru wa mazao ( Kata ya Oldonyosambu, Kata ya Bangata, Kata ya Kisongo, Kata ya Kiranyi na Kata ya Oljoro) | **LGA/007/2023/24/HQ/NC/02 LOT 8** |

**MUHIMU: Makusanyo yote ya mapato yatakusanywa kwa kutumia mfumo wa TAUSI.**

2. Unaalikwa kuwasilisha Zabuni yako kwa ajili ya kukusanya Mapato kama ilivy*oainishwa kwenye Nyaraka za Zabuni.*

3. Zabuni zote zikiwa zimejazwa kikamilifu ziwasilishwe Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kupitia TANePS kabla ya Tarehe **05/06/2023** Saa **NNE NA NUSU ASUBUHI**. Ufunguzi wa Zabuni hizo utafanyika kupitia TANePS mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha Zabuni.

4. Mzabuni anaruhusiwa kuomba Zabuni Zaidi ya moja kati ya hizo zilizoainishwa kwenye jedwali

5. Muombaji ataje kiasi (asilimia ya Comission atakayolipwa) na Halmashauri kati ya 1%-20%

6. Uthibitisho wa uwezo wa Muombaji kifedha kwa kuonesha taarifa ya Fedha ya Benki (Bank statement) ya mwaka mmoja hadi sasa 2022-2023,iliyoidhinishwa na kuthibitishwa na meneja wa benki husika.Halmashauri itawasiliana na Benk husika kwa uthibitisho.

7. Muombaji aoneshe mahali ofisi zake zilipo.Halmashauri itatembelea ofisi hizo

8. Mwombaji asiwe na deni au mgogoro wowote na Halmashauri ya wilaya ya Arusha. Aidha mwombaji aliyewahi kushitakiwa na Halmashauri ya Arusha kuhusiana na kazi ya ukusanyaji wa mapato kutoka vyanzo vyake hatapewa nafasi ya ushindani kwa kazi yoyote ya zabuni iliyotangazwa.

9. Iwapo itathibitika kuwa Mzabuni aliye na mgogoro na Halmashauri ametumia jina jingine la kampuni,kuomba kazi ya uwakala,zabuni hiyo haitapewa nafasi ya ushindani kwa kazi yoyote ya zabuni,Aidha Halmashauri itavunja mkataba kama hatua hiyo imekwishafikiwa.

10. Zabuni au sehemu za Zabuni ambazo zitawasilishwa kwa njia nyingine tofauti na TANePS au zilizowasilishwa katika muundo usiokubalika na TANePS, hazitakubaliwa wala kuzingatiwa kwa ajili ya tathmini, bila kujali mazingira yoyote.

***MKURUGENZI MTENDAJI***

***HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA***

## SEHEMUYA PILI: MAELEKEZO KWA WAZABUNI

| | |
|---|---|
| 1. | 1.1 Taasisi Nunuzi (TN) iliyotajwa katika Lohodata ya Zabuni (LDZ) inatangaza zabuni kwa ajili ya kukusanya mapato kama ilivyobainishwa kwenye **LDZ** na kwenye Jedwali la Mahitaji. Mzabuni Mshindi atatarajiwa kukusanya mapato mahali palipotajwa kwenye **LDZ** na katika kipindi kilichoainishwa kwenye **LDZ** kuanzia siku ambayo imetajwa kwenye **LDZ**. |
| 2. | 2.1 Serikali ya Tanzania inakusudia kukusanya mapato na inategemea kwamba sehemu za mapato hayo itatumika kumlipa mtoa huduma wa ukusanyaji wa mapato katika Zabuni iliyotajwa katika **LDZ** katika mwaka wa fedha uliotajwa katika **LDZ**. |
| 3. | 3.1 Mzabuni anaweza kuwa mtu Binafsi, Kampuni, Ushirika, Taasisi au Kikundi cha watu kilichosajiliwa kisheria au ushirika au ubia baina yao.Kwa suala la ushirika au ubia, washirika au wabia wote watawajibika kipekee au kwa pamoja katika utekelezaji mkataba. Washirika au wabia watachagua kiongozi wao ambaye atakuwa na mamlaka ya kufanya biashara kwa ajili na kwa niaba ya washirika au wabia wengine.<br><br>3.2 Uteuzi wa kiongozi wa ushirika au ubia utathibitishwa kwa kuwasilisha Hati ya Kiapo cha Mamlaka ya Kisheria iliyothibitishwa na kamishina wa viapo kwa taasisi nunuzi.<br><br>3.3 Makubaliano yoyote yaliyounda ushirika au ubia yaliyothibitishwa na kamishina wa viapo yatawasilishwa kwa TN kama sehemu ya zabuni.<br><br>3.4 Zabuni ya washirika au wabia inapaswa kuainisha majukumu ya kila mbia au mshirika katika mkataba unaopendekezwa. Na kila mzabuni atafanyiwa tathmini au kupekuliwa kulingana na mchango wake tu na wajibu wa kila mbia hautabadilishwa pasipo ridhaa ya kimaandishi ya TN.<br><br>3.5 Mwaliko wa zabuni hii ni kwa wazabuni wanaostahili ambao wametajwa kwenye **LDZ**.<br><br>3.6 Wazabuni watapaswa kutimiza matakwa ya leseni na usajili ya mamlaka za kisheria za Tanzania. Wazabuni wa nje ya nchi hawaruhusiwi kushiriki zabuni hii.<br><br>3.7 Mzabuni hatakiwi kuwa na mgongano wa kimasilahi. Wazabuni wote watakaobanika kuwa na mgongano wa kimasilahi watakosa sifa ya kushiriki Zabuni hii.<br><br>3.8 Mzabuni hatastahili kuomba au kushinda zabuni hii iwapo: –<br><br>(a) Mzabuni ametangazwa muflisi; |

| | |
|---|---|
| | (b) Malipo kwa Mzabuni yamesimamishwa kwa mujibu wa hukumu ya mahakama mbali na hukumu ya kutangaza kufilisika na itokanayo, kwa mujibu wa sheria za nchi, kupoteza kwa ujumla au sehemu haki ya kusimamia na kuondosha mali zake;<br><br>(c) Michakato ya kisheria imeanzishwa dhidi ya mzabuni inayohusisha agizo la kusimamisha malipo na inayoweza kupelekea, kwa mujibu wa sheria za nchi, kutangazwa kufilisika au katika hali nyingine yeyote itakayopelekea kupoteza kwa ujumla au sehemu haki ya kusimamia na kuondosha mali;<br><br>(d) Mzabuni amehukumiwa kwa hukumu ya mwisho, ya kosa lolote linalohusisha maadili ya kitaalamu;<br><br>(e) Mzabuni amefungiwa au amekosa sifa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura ya 410 na Kanuni zake za Mwaka 2013, kushiriki katika ununuzi wa umma kwa ajili ya vitendo vya rushwa, kulazimisha maamuzi, kula njama, udanganyifu, kushindwa kuheshimu tamko la dhamana ya zabuni, kukiuka mkataba wa Ununuzi, kuwasilisha sifa za uongo katika mchakato wa Zabuni au vigezo vingine vitakavyoonekana vinafaa na Mamlaka au kampuni imepatikana na kosa la udanganyifu wa taarifa zilizohitajika kwa ajili ya ushiriki katika mwaliko wa zabuni.<br><br>3.9 Mashirika ya Umma au mashirika yanayomilikiwa kati ya Umma na makampuni binafsi yanaweza kushiriki katika zabuni hii, iwapo tu wameruhusiwa kisheria na wanajitegemea kifedha, kama wanafanyakazi chini ya sheria ya biashara, siyo wakala zinazoitegemea Serikali na wamesajiliwa na bodi au mamlaka husika.<br><br>3.10 Wazabuni watawasilisha kwa TN uthibitisho wa sifa zao, uthibitisho wa kukidhi matakwa muhimu ya kisheria, kiufundi na kifedha na uwezo wao na utoshelevu wa rasilimali za kutekeleza mkataba kwa ufanisi.<br><br>3.11 Wazabuni watawasilisha uthibitisho wa sifa zao endelevu kwa kiwango cha kuiridhisha TN, kama TN itakavyowaomba. |
| 4. | 4.1 Mzabuni ataambatisha nyaraka zifuatazo katika Zabuni:<br><br>(a) Nyaraka za usajili wa Mzabuni (mf. kikundi, kampuni n.k.)<br><br>(b) Fomu ya Zabuni iliyojazwa na kusainiwa ipasavyo;<br><br>(c) Jedwali la Mahitaji na Bei lililo katika **Sehemu ya Nne.** lililojazwa na kusainiwa ipasavyo; |

| | |
|---|---|
| | (d) Leseni halali ya Biashara;<br><br>(e) Hati Halali ya Usajili wa VAT (*kama ipo*);<br><br>(f) Cheti Safi ya Mlipakodi (Tax Clearance Certificate);<br><br>(g) Orodha ya mikataba iliyotekelezwa ndani ya muda utakaotajwa na TN kwenye **LDZ**, inayojumuisha majina na anuani za taasisi zilizopokea huduma hizo, kwa ajili ya uthibitisho kama itakavyoainishwa na TN kwenye **LDZ**;<br><br>(h) Tamko la Dhamana ya Zabuni*;*<br><br>(i) Hati ya Kiapo cha Mamlaka ya Kisheria iliyoidhinishwa (*isipokuwa kwa kampuni linalomilikiwa na mtu mmoja (sole proprietor));*<br><br>(j) Fomu ya Uadilifu iliyo katika Nyaraka za Zabuni iliyojazwa na kusainiwa;<br><br>(k) Nyaraka nyinginezo zote zitakazohitajika na Taasisi Nunuzi kama zilivyotajwa kwenye Lohodata ya Zabuni (**LDZ**) |
| 5. | 5. Taarifa za mahitaji zimeambatanishwa katika **Sehemu ya Tano.** |
| 6. | Bei ya Zabuni;<br><br>6.1 Mkataba utakuwa ni wa utoaji wa Huduma kulingana na mahitaji yote yaliyoainishwa katika Jedwali la Mahitaji na Bei**;**<br><br>6.2 Marekebisho yoyote, kama yatakuwepo, yanaweza kufanyika kwa kubadilisha zabuni ambayo imekwisha wasilishwa muda wowote kabla ya muda wa mwisho wa kuwasilisha zabuni kupitia TANePS. Aidha, marekebisho yanaweza pia kufanyika kwa kukata sehemu husika, kuweka saini ya mtu aliyeidhinishwa, tarehe na kuandika kwa usahihi kabla kuwasilisha nyaraka kupitia TANePS, muda wowote kabla ya muda wa mwisho wa kuwasilisha zabuni;<br><br>6.3 Bei ya zabuni itajumuisha ushuru wote, kodi na ada anazotakiwa kulipa Mzabuni katika Mkataba;<br><br>6.4 Vizio vya kima (unit rates) vilivyotajwa na Mzabuni na kukubalika na pande zote za mkataba, havitabadilika katika kipindi chote cha utekelezaji wa mkataba.<br><br>6.5 Bei zinapaswa kunukuliwa katika Shilingi ya Tanzania (TZS). |

| | |
|---|---|
| 7. | Mzabuni atakamilisha kujaza Fomu ya Kuwasilishia Zabuni ambayo imeambatanishwa katika **Sehemu ya Nane.** Fomu ya Kuwasilisha Zabuni itajazwa kikamilifu bila ya mabadiliko katika muundo wake na hakuna fomu mbadala itakayokubaliwa. |
| 8. | Malipo yatafanywa katika Shilingi ya Tanzania (TZS). |
| 9. | Zabuni zitabaki kuwa hai kwa siku [*andika siku zisizozidi 120]* baada ya siku ya mwisho ya uwasilishaji Zabuni. |
| 10. | 10.1 Zabuni zote zikiwa zimejazwa kikamilifu ziwasilishwe kwenye taasisi ambayo imetajwa kwenye **LDZ** kupitia TANePS kabla ya tarehe, siku na muda uliotajwa kwenye LDZ. Ufunguzi wa Zabuni hizo utafanyika kupitia TANePS mara baada ya muda wa mwisho wa kuwasilisha Zabuni. |
| 11. | Endapo itaainishwa kwenye **LDZ**, Mzabuni anaweza kuwasilisha Zabuni mbadala. |
| 12. | 12.1 Isipokuwa kwa kampuni linalomilikiwa na mtu mmoja *(sole proprietor)*, Zabuni itakamilishwa na kusainiwa na mwakilishi aliyeidhinishwa na Mzabuni. Kwa muktadha huu, Hati ya Kiapo cha Mamlaka ya Kisheria itawasilishwa pamoja na Zabuni<br><br>12.2 Kwa sole proprietor, atatakiwa kuwasilisha nakala ya kitambulisho iliyoidhinishwa na mwakilishi wa Kamishna wa Viapo. |
| 13. | TN itafanyia tathmini na kulinganisha Zabuni kwa namna ifuatayo:<br><br>13.1 Tathmini ya Awali; ilikutambua ni Zabuni zipi zinakidhi matakwa ya msingi ya nyaraka za Zabuni, kama vile: zilezilizosainiwa kwa usahihi na zilizotimiza vigezo na masharti ya Mwaliko wa Zabuni.<br><br>i) Vigezo vifuatavyo vitaangaliwa wakati wa tathmini ya awali:<br><br>a) Nyaraka za usajili wa Mzabuni (mf. kikundi, kampuni n.k.)<br><br>b) Leseni halali ya Biashara;<br><br>c) Cheti Halali Usajili wa VAT (*kama ipo*)<br><br>d) Cheti Safi cha Mlipakodi (Tax Clearance Certificate);<br><br>e) Fomu ya kuwasilisha zabuni yenye bei iliyojazwa kikamilifu na kusainiwa ipasavyo sambamba na Jedwali la Mahitaji na Bei;<br><br>f) Tamko la Dhamana ya Zabuni*;*<br><br>g) Hati Sanifu ya Kiapo cha Mamlaka ya Kisheria iliyoidhinishwa (*isipokuwa* |

*kwa kampuni linalomilikiwa na mtu mmoja (sole proprietor);*

h) Fomu ya Uadilifu iliyo katika Sehemu ya Nane iliyojazwa na kusainiwa;

i) Uwezo/utayari wa Mzabuni kuwasilisha mapato ndani ya muda uliowekwa kwenye **LDZ**;

j) nyaraka nyingine zozote zitakazohitajika na TN kama zilivyotajwa kwenye Lohodata ya Zabuni (**LDZ**)

ii) Kama sehemu ya tathmini ya awali, TN itaangalia:

(a) Orodha ya mikataba iliyotekelezwa karibuni inayojumuisha majina na anuani za taasisi zilizopokea huduma kwa ajili ya uthibitisho;

(b) Uwezo wa kifedha;

(c) Vigezo vingine vya muhimu ambavyo TN itaona vinahitajika vitatajwa kwenye **LDZ**

Angalizo: Kukosekana kwa kigezo kimojawapo kati ya hivyo vilivyotajwa hapo juu, au kubadili maneno ya fomu sanifu zilizoambatanishwa kwenye nyaraka hizi kutasababisha Mzabuni kuenguliwa kwenye hatua hii ya tathmini ya awali.

13.2 Zabuni zitakazokidhi matakwa ya Nyaraka za Zabuni zitafanyiwa Tathmini ya Kina kwa;

(a) Kufanya marekebisho ya makosa ya kihesabu: kama kutakuwa na tofauti ya kimahesabu kati ya kizio cha kima (unit rate) na kiasi (sub-total amount) kilichowasilishwa, basi kizio cha kima kitatumika katika tathimini ya Zabuni na katika Makubaliano ya Mkataba utakaofuata.

(b) Kufanya marekebisho stahili, kwa ajili ya mabadiliko yanayokubalika, (variations, deviations) au mabadiliko yanayotokana na kutowekwa kwa baadhi ya vipengele;

(c) Kufanya marekebisho stahili kuakisi punguzo la bei ya tuzo au marekebisho mengine ya bei yaliyotolewa;

13.3 Ulinganishaji wa Zabuni; Katika kulinganisha Zabuni, kamati ya tathmini itaweka kwa kila Mzabuni bei ya Zabuni iliyofanyiwa tathmini ili kubaini Mzabuni mwenye bei kubwa.

13.4 Mzabuni atakayeoneka na kuwa na bei kubwa baada ya kufanyiwa tathmini,

| | |
|---|---|
| | atafanyiwa uhakiki wa uwezo na sifa ili kujiridhisha kwamba ataweza kuingia mkataba na kutekeleza majukumu yake ya mkataba kwa ufanisi. |
| 14. | **TN** itatoa tuzo ya mkataba kwa Mzabuni ambaye Zabuni yake imeonekana kukidhi vigezo vya Zabuni na ambayo imewasilisha bei ya Zabuni iliyofanyiwa tathmini na kuwa na bei kubwa zaidi. |
| 15. | Bila ya kuathiri yaliyotajwa hapo juu, TN inayo haki ya kukubali au kukataa Zabuni zote muda wowote kabla ya kutoa tuzo ya Mkataba. |
| 16. | Kabla ya kutoa tuzo ya Mkataba, TN itatoa Barua ya Kusudio la kutoa Tuzo kwa Wazabuni wote walioshiriki katika zabuni hiyo ikitoa siku saba za kazi kwa Wazabuni hao kuwasilisha malalamiko yoyote (kama yatakuwepo kupitia TANePS. Endapo Mzabuni hatoridhika na maamuzi ya TN, anaweza kukata rufaa kwenye Mamlaka ya Rufaa za Zabuni (PPAA). |
| 17. | Mzabuni ambaye Zabuni yake imekubaliwa atajulishwa na TN kuwa amekubaliwa kupewa tuzo ya mkataba kabla ya kuisha kwa kipindi cha uhai wa Zabuni. |
| 18. | 18.1 Mzabuni mshindi atatakiwa kuwasilisha Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba ndani ya siku kumi na nne (14) za kazi baada ya kukamilika masharti ya kabla ya kusaini mkataba, baada yakupokea barua ya tuzo na kabla ya kusainiwa kwa mkataba. Kiwango na aina ya dhamana hiyo vitatajwa kwenye **LDZ** na **MMM**.<br><br>18.2 Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba itakuwa kwa fedha ya Tanzania katika aina mojawapo kati hizi zifuatazo:<br><br>(a) Dhamana ya benki au barua ya mkopo iliyotolewa na benki iliyo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayokubalika kwa Mnunuzi, katika muundo uliotolewa katika Mwaliko wa Zabuni au muundo mwingine unaokubalika na Mnunuzi; au<br><br>(b) Fedha taslimu, hundi halali; au<br><br>(c) Dhamana ya bima; au<br><br>(d) Aina nyingine ya dhamana itakayokubalika na Mnunuzi. |
| 19. | Wazabuni wana haki ya kuomba mapitio ya maamuzi ya mchakato wa ununuzi kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura namba 410 na Kanuni zake za mwaka 2013 kwenye anuani ya taasisi nunuzi au Mamlaka ya Rufaa za Zabuni (PPAA) ambayo imetolewa kwenye **LDZ** na nakala ya malalamiko itumwe PPRA kwenye anuani |

| | |
|---|---|
| | iliyotolewa kwenye **LDZ** |

## SEHEMU YA TATU: LOHODATA YA ZABUNI (LDZ)

| LDZ | MKW | Maboresho, Mapendekezo, Nyongeza ya Vifungu vya MKW |
|---|---|---|
| 1.0 | 1.1 | Jina la TN: Halmashauri ya Wilaya ya Arusha<br>Huduma zitakazonunuliwa ni: **ZABUNI YA KUWAPATA MAWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA KATIKA VYANZO VYAKE MBALIMBALI kama ifuatavyo:**<br>• Ushuru wa madini ya ujenzi geti la Mbuyuni kata ya oljoro<br>• Ushuru wa masoko ya Mirongoine,Olokii,Oldonyowas,Ngaramtoni,Kisongo<br>• Ushuru wa Moram Nyeupe Oldonyosambu<br>• Ushuru wa Maegesho<br>• Ushuru wa choo soko la Ngaramtoni na Oldonyowas<br>• Ushuru wa Moram Kisongo<br>• Ushuru wa Mkaa na mazao ya misitu geti la Kisongo<br>• Ushuru wa mazao ( Kata ya Oldonyosambu, Kata ya Bangata, Kata ya Kisongo, Kata ya Kiranyi na Kata ya Oljoro)<br>Muda/kipindi cha uwasilishaji wa Huduma: **01.07.2023 hadi tarehe 30.06.2024**<br>Tarehe ya kuanza utekelezaji wa mkataba itakuwa **01.07.2023** |
| 2.0 | 2.1 | Mwaka wa Fedha: **2023/2024**<br>Jina la Mradi: ZABUNI YA KUWAPATA MAWAKALA WA KUKUSANYA MAPATO KATIKA VYONZO MBALIMBALI VYA HALIMASHAURI<br>**LGA-007/2023-2024/HQ/NC/01** |
| 3.0 | 3.5 | Wazabuni wanaostahili kushiriki ni: Mtu Binafsi, Kampuni, Ushirika, Taasisi au Kikundi cha watu kilichosajiliwa kisheria au ushirika au ubia baina yao. Kwa suala la ushirika au ubia, washirika au wabia wote watawajibika kipekee au kwa pamoja katika utekelezaji mkataba. Washirika au wabia watachagua kiongozi wao ambaye atakuwa na mamlaka ya kufanya biashara kwa ajili na kwa niaba ya washirika au wabia wengine. |

| | | |
|---|---|---|
| | | Ukomo wa juu wa Washirika wa pamoja na wabia itakuwa ni: ***HAIHUSIK**I* |
| 4.0 | 9.1&9.2 | Zabuni itakuwa hai kwa muda wa siku **120** |
| 5.0 | 10.1 | Halmashauri Ya Wilaya Arusha<br>Tarehe ya mwisho ya kuwasilisha zabuni ni:<br>*Tarehe:* ***05.06.2022***<br>*siku:* ***JUMATATU***<br>*Muda:* ***SAA NNE NA NUSU ASUBUHI*** |
| 6.0 | 11 | Zabuni Mbadala *"hazikubaliki"* |
| 7.0 | 13.1.(j) na 13.1(d) | Nyaraka ambazo Taasisi nunuzi itatumia wakati wa tathmini ni<br>• Nyaraka za usajili wa Mzabuni (mf. kikundi, kampuni n.k.)<br>• Leseni halali ya Biashara;<br>• Cheti Halali Usajili wa VAT (kama ipo)<br>• Cheti Safi cha Mlipakodi (Tax Clearance Certificate);<br>• Fomu ya kuwasilisha zabuni yenye bei iliyojazwa kikamilifu na kusainiwa ipasavyo sambamba na Jedwali la Mahitaji na Bei;<br>• Tamko la Dhamana ya Zabuni; (tender declaration)<br>• Hati Sanifu ya Kiapo cha Mamlaka ya Kisheria iliyoidhinishwa (power of attorney) isipokuwa kwa kampuni linalomilikiwa na mtu mmoja (sole proprietor);<br>• Fomu ya Uadilifu iliyo katika Sehemu ya Nane iliyojazwa na kusainiwa;<br>• Uthibitisho wa uwezo wa Muombaji kifedha kwa kuonesha taarifa ya Fedha ya Benki (Bank statement) ya mwaka mmoja hadi sasa 2022-2023 Halmashhauri itafanya uthibitisho kutoka benk husika<br>• Maelezo ya kazi alizowahi kufanya na uzoefu usiopungua mwaka mmoja wa huduma ya uwakala na ukusanyaji wa mapato. **Ambatanisha mkataba**.<br>• Muombaji ataje kiasi (asilimia ya Comission atakayolipwa) na Halmashauri<br>• Mwombaji asiwe na deni au mgogoro wowote na Halmashauri ya Wilaya ya Arusha. Aidha **MZABUNI ALIYE NA DENI** NA Taasisi yoyote ya Serikali ataondolewa katika Zabuni. |
| 8.0 | 17.1 | Kiwango cha Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba: Mzabuni mshindi atatakiwa kuwasilisha Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba ndani ya siku |

| | | |
|---|---|---|
| | | kumi na nne (14) za kazi baada ya kukamilika masharti ya kabla ya kusaini mkataba, baada yakupokea barua ya tuzo na kabla ya kusainiwa kwa mkataba.<br>Aina ya Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba:<br>• Dhamana ya benki au barua ya mkopo iliyotolewa na benki iliyo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayokubalika kwa Mnunuzi, katika muundo uliotolewa katika Mwaliko wa Zabuni au muundo mwingine unaokubalika na Mnunuzi; au<br>• Fedha taslimu, hundi halali; au<br>• Dhamana ya bima; |
| | | Kiwango cha juu cha Malipo ya awali kitakuwa HAIHUSIKI |
| | 18 | Mkurugenzi mtendaji,<br>Halmashauri ya wilaya ya Arusha,<br>S.L.P 2330,<br>**ARUSHA**<br>**Anuani ya PPAA:**<br>Katibu Mtendaji,<br>Mamlaka ya Rufaa za Zabuni,<br>S. L. P 9310,<br>**DAR ES SALAAM**<br>**Anuani ya PPRA kwa ajili ya Nakala:**<br>Afisa Mtendaji Mkuu,<br>Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma,<br>Ghorofa ya 9, Jengo la Kambarage, Barabara ya PSPF,<br>S. L. P 2865,<br>41104 **DODOMA**. |

## SEHEMU YA NNE; JEDWALI LA BEI

| Maelezo ya Huduma | Idadi yamakadirio | Kima/tozo | Kiasi (TZS) | ASILIMIA YA UREJESHAJI % |
|---|---|---|---|---|
| **USHURU WA MADINI YA UJENZI GETI LA MBUYUNI KATA YA OLJORO** | | | | |
| **USHURU WA MORAM NYEUPE OLDONYOSAMBU** | | | | |
| **USHURU WA MASOKO MIRONGOINE,OLOKII ,OLDONYOSAMBU,NGARAMTON,KISONGO** | | | | |
| **USHURU WA MAEGESHO** | | | | |
| **USHURU WA CHOO NGARAMTON** | | | | |
| **USHURU WA CHOO SOKO LA OLDONYOWAS** | | | | |
| **USHURU WA MORAM KISONGO** | | | | |

## SEHEMU YA TISA: FOMU

*[Ingiza karatasi ya Anuani chapwa ya Mzabuni, Anwani Kamili ya Posta, na simu, fasimili na namba ya teleksi na anwani ya Barua pepe]*

## 1. Fomu ya Kuwasilisha Zabuni

M/s [*Ingiza Jina na Anuani ya Mzabuni*]

*Tarehe:*

Kwa: ……………………………………….

………………………………………..

…………………………………………

Baada ya kupitia Nyaraka ya Zabuni na nyongeza yake [ingiza namba ya nyongeza (kama ipo)], Sisi, tunakubali kutoa Huduma ya [*ingiza maelezo ya huduma ya ukusanyaji mapato, na namba ya utambulisho wa zabuni*] kwa mujibu wa Masharti ya Mkataba yanayoambatana na Zabuni hii kwa jumla ya Bei ya Mkataba ya *[ingiza kiasi kwa maneno, tarakimu na aina ya sarafu/fedha],* katika Shilingi za Tanzania au kwa jumla ya bei itakayobainishwa kulingana na Jedwali la Mahitaji na Bei lililoambatanishwa kama sehemu ya Zabuni hii.

Tunaafiki uteuzi wa [*ingiza jina la msuluhishi pendekezwa*] kuwa Msuluhishi wetu katika migogoro yoyote itakayojitokeza wakati wa Mkataba.

**Au**

Hatuafiki uteuzi wa [*ingiza jina la msuluhishi pendekezwa*] kuwa Msuluhishi, na tunampendekeza [*ingiza jina la msuluhishi mbadala*] kama mbadala wake, ambaye ada yake kwa siku na sifa zake zimeambatanishwa.

Kama Zabuni yetu itakubaliwa, tunaahidi kuwasilisha Huduma husika zilizotajwa ndani ya kipindi cha [] [*ingiza idadi ya* siku/wiki/miezi *(futa isiyohusika)*] kama ilivyoainishwa katika ALU, Masharti Maalumu ya Mkataba na katika Masharti ya Jumla ya Mkataba.

Endapo, Zabuni yetu itakubaliwa, tuko tayari kuwasilisha [*Dhamana ya Utekelezaji Kazi au Tamko la Dhamana ya Utekelezaji Kazi (futa isiyohusika)*] kama lilivyoanishwa kwenye Nyaraka za Zabuni.

Zabuni hii, barua yako ya kukubali, pamoja na Agizo la Ununuzi vitaunda mkataba unaotufunga kisheria baada ya kusainiwa kwa Mkataba. Tunafahamu kuwa hulazimiki

kukubali Zabuni yenye bei ndogo au Zabuni nyingine yoyote kati ya Zabuni unazopokea.

Tunakubali kufungwa na Zabuni hii kwa Kipindi chote cha Uhai wa Zabuni kilichoainishwa katika MKW 6 na itatufunga na inaweza kukubaliwa muda wowote kabla yaukomo wa uhai wa Zabuni.

Hatushiriki katika Zabuni zaidi ya moja kama Wazabuni katika mchakato huu, tofauti na Zabuni mbadala kwa mujibu wa Nyaraka za Mwaliko wa Zabuni.

Tunathibitisha kwamba Bei ya Zabuni haikuhusisha makubaliano na Wazabuni wengine kwa madhumuni ya kuharibu Ushindani katika Zabuni.

Tunathibitisha kwamba Zabuni hii inazingatia Masharti yaliyotakiwa na Mwaliko wa Zabuni.

Saini Iliyoidhinishwa: …………………………………………………………………

Jina na Cheo cha Mweka Sahihi: ……………………………………………......

Tarehe……………………………………………………………………………….

Jina la Mzabuni: ……………………………………………………………………

**Anuani:** ………………………………………………………………………………..

## 2. Tamko la Dhamana ya Zabuni

Tarehe: *[ingiza tarehe (siku, mwezi na mwaka]*

Namba ya Zabuni: **LGA-007/2023-2024/HQ/NC/01**

Namba Mbadala: *[ingiza namba ya utambulisho, iwapo Zabuni hii ni mbadala]*

Kwa: **Halmashauri Ya Wilaya Arusha**

Sisi, watia saini, tunatoa tamko kuwa:

Tunafahamu kwamba, kwa mujibu wa masharti yako, Zabuni lazima iwasilishwe na Tamko la Dhamana ya Zabuni.

Tunakubali kuwa, tutazuiliwa kushiriki katika ununzi wa umma kwa kipindi cha muda utakaoamuliwa na Mamlaka, iwapo tutakuwa tumevunja makubaliano yaliyomo katika masharti ya Zabuni, kwa sababu:

(a) tumeondoa au kubadilisha Zabuni yetu ndani ya kipindi cha Uhai wa Zabuni ulioainishwa katika Fomu ya Zabuni;

(b) hatutakubaliana na masahihisho ya kihesabu yaliofanyika katika bei ya Zabuni; au

(c) tukiwa tumejulishwa juu ya kukubaliwa kwa Zabuni yetu na TN katika kipindi cha Muda wa Uhai wa Zabuni:

i. kushindwa kusaini mkataba pale TN atakapohitaji hivyo; au

ii. Kushindwa au kukataa kutoa Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba au kutekeleza masharti mengine yoyote yanayoendana na usainishaji wa mkataba kama ilivyobainishwa katika Nyaraka za Zabuni.

Tunafahamu kuwa, Tamko hili la Dhamana ya Zabuni litaisha muda wake iwapo hatutakuwa Mzabuni Mshindi, mpaka pale ambapo chochote kati ya vifuatavyo kitaanza: (i) tutakapopokea Taarifa ya Barua ya Tuzo itakayokuwa na Mzabuni Mshindi; au (ii) siku ishirini na nane (28) baada ya ukomo wa mwisho wa Zabuni yetu.

Saini: *[ingiza saini ya mtu ambaye jina na uwezo wake umeobainishwa]*

Katika uwezo wa *[ingiza uwezo wa kisheria wa mtu wa kusaini Tamko la Dhamana ya Zabuni]*

Jina: *[Ingiza jina kamili la mtu wa kusainiTamko la Dhamana ya Zabuni]*

Aliyeidhinishwa kusaini Zabuni kwa niaba ya *[Ingiza jina kamili la Mzabuni]*

Tarehe _____________ siku ya _______________, ________ *[ingiza tarehe ya kusaini]*

Muhuri wa Kampuni (inapofaa)

**Halmashauri Ya Wilaya Ya Arusha.**

## 3. Barua ya Kukubali Kotesheni

Kwa **……………………………………………..........................***(Andika jina na anuani ya Mzabuni/Zabuni)*

Hii ni kukutaarifu kuwa kotesheni yako ya tarehe *[Ingiza tarehe]* ya kufanya kazi ya [*Ingiza maelezo ya kazi, jina la Mkandarasi na namba ya utambulisho kama ilivyoonyeshwa kwenye nyaraka za kotesheni]* kwa bei ya Mkataba wa shilingi za Tanzania *[Ingiza kiasi kwa maneno, tarakimu na sarafu]*, kama ilivyosahihishwa na kurekebishwa kulingana na maelekezo ya mwaliko wa kotesheni imekubaliwa.

Unatakiwa kuwasilisha Tamko la Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba ndani ya siku 14 za kazi baada ya kupokea Barua hii ya Tuzo kabla ya kusaini Mkataba. Aidha, Unatakiwa kuweka saini makubaliano ya Mkataba katika ofisi hii tarehe [*Ingiza tarehe*] muda wa [*Ingiza muda*] .

Sahihi Idhinishwa: ……………………………......…………………………….…

Jina na Cheo cha Mweka Sahihi: ……………………………………………...………

Jina la Mwajiri: …………………………………...…………………………………

### 4. Tamko la Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba[1]

Tarehe: *[ingiza tarehe (siku: mwezi: mwaka)]*

Na. ya Mkataba: **LGA-007/2023-2024/HQ/NC/01**

Kwa: *[Ingiza Jina kamili la Mwajiri]*

Sisi, watia saini hapo chini, tunatamka kwamba:

1. Tunafahamu kwamba,kwa mujibu wa masharti yako, tunatakiwa kuhakikisha utekelezaji wa Mkataba tajwa hapo juu kwa uaminifu kama tutakavyokubaliana, kwamba tutawasilisha Tamko la Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba huo ndani ya siku 14 za kazi tangu kupokea barua yako ya kukubali zabuni yetu na kabla ya kusaini Mkataba husika.

2. Tunafahamu na kukubali kwamba: sisi tutapoteza sifa ya kushiriki kwenye zabuni za umma kwa kipindi ambacho kitatajwa na Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma endapo tutashindwa kutekeleza majukumu yetu chini ya Mkataba tajwa hapo juu kwa mujibu wa taratibu za kufungia wazabuni zilizoainishwa kwenye Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake.

Tunatambua kwamba Tamko hili la Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba halitakuwa na uhalali juu yetu pale ambapo Mwajiri ataridhika na utendaji wetu wa kazi na kutoa hati ya mwisho ya kumaliza kazi katika Mkataba huo.

Imesainiwa: [*ingiza Saini ya mtu aliyepewa Mamlaka*]
Nafasi ya Kisheria [ingiza nafasi ya kisheria ya mtu aliyepewa mamlaka]

Jina: *[ingiza jina kamili la mtu aliyepewa Mamlaka ya Kusaini Tamko]*

Nimepewa mamlaka ya Kusaini Tamko hili kwa niaba ya: *[ingiza jina la Mkandarasi]* [*ingiza tarehe*, mwezi na *mwaka wa Hati ya Kiapo ya Mamlaka ya Kisheria*]

*[ingiza tarehe ya kusaini Tamko la Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba]*

Muhuri wa ofisi/kikundi

---

[1] Hutumika Kama mbadala wa Dhamana ya Utekelezaji wa Mkataba kwa Mikataba iliyo ndani ya viwango vya Upendeleo Maalum wa. Inapaswa kuwasilisha ndani ya siku 14 za kazi baada ya mzabuni kupokea tuzo

### 5. Hati Mahsusi ya Mamlaka ya Kiapo cha Kisheria (PoA)

Sisi ambao saini zetu zimeoneshwa hapa chini*………………………… [Jina la Kampuni/ Mtoa Idhini]* wa *………….[anuani ya kampuni/mtoaidhini],* kwa mamlaka tuliyopewa ya azimio ya Bodi ya Wakurugenzi Na. *…….* ya tarehe …………..mwezi……….mwaka …….. ……….

Tunamteua na kumuidhinisha Ndugu *…………..[Taja jina la mpewa idhini]* kuwa mwakilishi wetu halali kisheria akiwa na mamlaka kamili kwa niaba yetu na kwa majina yetu na kwa maslahi na faida yetu kufanya moja au yote kati ya haya yafuatayo katika kutekeleza Zabuni Na……….. [*taja namba ya zabuni*]; Hii ikimaanisha kufanya jambo lolote kwa niaba ya kampuni na kufanya jambo lolote linalohusiana na Zabuni Na………………[*ingiza namba ya zabuni*] inayohusu……………..[*taja jina la zabuni*] kwa ya taasisi ………………..[*ingiza jina la taasisi nunuzi*].

**NA KWAMBA** hati hii sanifu ya mamlaka ya kisheria haitabatilisha au kuathiri hati sanifu yoyote ya nguvu ya kisheria itakayotolewa kwa mtu yeyote au watu wengine wowote kwa mamlaka ya aina hiyo na kwamba mamlaka hayo yatabaki kuwa na nguvu na mamlaka kana kwamba hati hii haijatolewa.

**NA KWAMBA** tunaidhinisha kitu chochote ambacho mwakilishi wetu, wakala au mbadala wake atakayemteua kwa mamlaka yake atakachokifanya kwa mamlaka yake katika kutekeleza au kukusudia kutekeleza kwa kuzingatia mamlaka ya hati hii sanifu ya nguvu ya kisheria.

Imewekwa lakiri ya kamapuni …………………….. [*ingiza jina la kampuni*] na imetolewa mbele yetu leo hii tarehe …………………mwezi ………….. mwaka ……………….

**KWA USHUHUDA** makubaliano haya yamesainiwa leo tarehe ………………..mwezi ………………… mwaka …………………. hapa …………………. [*Mahali*] kwa niaba ya ………………………[*ingiza jina la kampuni*] .

Imewekwa nakiri na kutolewa hapa ……………..………..……….
[*taja mahali*] na …………………………… [*ingiza jina la mtoa idhini*] ……………..
Ambaye ninamfahamu/ametambulishwa na …………….………… **MTOA IDHINI**
Ambaye ninamfahamu leo tarehe ………mwezi …….mwaka ………

**MBELE YANGU:**

**Jina: ...........................................................................**

**Saini: .........................................................................**

**Wadhifa: ………………………………………………**

Imesainiwa na kupokelewa hapa ………………………………….
[*taja mahali*] na ……………………… [*ingiza jina la mpokea idhini*] …………………
Ambaye ninamfahamu/ametambulishwa na …..……………..……… **MPOKEA IDHINI**
Ambaye ninamfahamu leo tarehe …..… mwezi …… mwaka …….

**MBELE YANGU:**

**Jina: ...........................................................................**

**Saini: ............................................................................**

**Wadhifa: ……………………………………………...**

## SEHEMU YA KUMI: UADILIFU

**SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**AHADI YA MTOA HUDUMA KUHUSU SERA DHIDI YA RUSHWA, KANUNI ZA MAADILINA PROGRAMU YA UKIDHI**

Sisi [*ingiza jina la Mtoa Huduma]* tunaweka umuhimu katika zabuni ya ushindani unaofanyika kwa misingi ya haki, uhuru na isiyoruhusu unyanyasaji. Tunapenda kuthibitisha kuwa hatutatoa wala kuwezesha moja kwa moja au vinginevyo, ushawishi wowote usiofaa au zawadi kwa afisa yeyote wa umma, ndugu zake au watu wenye uhusiano wa kibiashara, inayohusu Zabuni hii, au utekelezaji unaofuata wa mkataba iwapo tutashinda.

Tunayo Sera Dhidi ya Rushwa /Kanuni za Maadili na Programu ya Kukidhi Masharti inayojumuisha hatua zote za maana na muhimu kuhakikisha kuwa ahadi yetu ya kutotoa rushwa iliyotolewa katika maelezo haya itazingatiwa na menejimenti yetu na waajiriwa pamoja na watu wengine wote (third parties) wanaofanyakazi na sisi katika miradi ya sekta ya umma au mkataba ikiwa ni pamoja na mawakala, washauri-elekezi, wabia wetu, Wauzaji wa Mikataba Midogo na wauzaji wetu. Nakala zetu za Sera Dhidi ya Rushwa /Kanuni za Maadili na Programu ya Kukidhi Masharti zimeambatanishwa.

| ______________________________ | _______________ | _____________ |
|---|---|---|
| *(Jina la mtu aliyepewa mamlaka)* | *Sahihi* | *Tarehe* |

________________________

*Muhuri/ Alama ya Kampuni*